# UANAFUNZI




Shemeji Melayeki

*Global Family Gatherings Ministries*


“God’s Standards”

UANAFUNZI © 2021 Shemeji Melayeki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.

SIMU: +255 714 548 565

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*

YouTube: Apostle *Shemeji Melayeki*

Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*

Twitter: *@melayeki*

Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

# YALIYOMO

UTANGULIZI .................................................................... iv

KWA NINI UWAFANYE WENGINE KUWA WANAFUNZI? ............... 1

PATA MUDA KUELEZEA KUTOKA KWENYE MAANDIKO ................ 3

UANAFUNZI NI MAHUSIANO .................................................. 9

SIYO UBUNIFU, NI MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI........................ 13

KUAMUA KUHUBIRI KWELI NI KUAMUA KUTOHUBIRI KITU KINGINE .................................................................... 23

WAAMBIE WATU WOTE UJUMBE HUO HUO............................. 33

HAINA MAANA WOTE WATAKUBALI ........................................ 45

MWISHO .................................................................... 56

# UTANGULIZI

Agizo kuu au Great Commission kama ambavyo wengi wamezoea kuita kwa kingereza ni mpango wa Mungu kuendeleza yale ambayo Yesu amefanya kwa ajili ya ulimwengu wote na kufundisha kwa wanafunzi wake ili kwamba nao wawafundishe watu wengine ambao nao watawafundisha watu wengine na hatimaye kila mtu kupata ujumbe uliokusudiwa. Agizo hili limewekwa wazi katika vitabu vine vya injili. Tuanze na Marko…

Marko 16:15-18

[15]Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, MKAIHUBIRI INJILI KWA KILA KIUMBE.

[16]Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.

[17]Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

[18]watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.

**Mkaihubiri** kwa **kila kiumbe**. Mara nyingi watu huchanganya kuhubiri na kufundisha kama vile ni kama vitu viwili vinavyotofautiana kabisa. Lakini maneno yote mawili yanahusiana na kupeleka habari njema za upendo wa Mungu kwa watu. Ndiyo maana habari hiyo hiyo Mathayo anaita na KUWAFUNDISHA KUYASHIKA YOTE NILIYOWAAMURU.

Mathayo 28:18-20

[18]Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

[19]Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa WANAFUNZI, MKIWABATIZA kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;

[20]na KUWAFUNDISHA KUYASHIKA YOTE NILIYOWAAMURU ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Maneno kila kiumbe pia yamechukuliwa tofauti, wengine wakafikiri kila kiumbe (zaidi ya mwanadamu) anahitaji Injili. Lakini si kweli kabisa. Yasu alikuja kwa ajili ya watu. Mathayo 1:21
[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye **ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.**

Ndiyo maana maelezo ya Mathayo ya Agizo Kuu anasema BASI, ENENDENI, MKAWAFANYE MATAIFA YOTE KUWA WANAFUNZI. Mataifa ni watu siyo mbuzi na kondoo.
Je, haya yote ni yapi?
Agizo hili limeandikwa pia na Luka. Na Luka atatuonyesha haya yote..

Luka 24:46-47
[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;
[47]na kwamba mataifa yote WATAHUBIRIWA kwa JINA LAKE lake habari ya TOBA na ONDOLEO la DHAMBI, kuanza tangu Yerusalemu.
Kwa hiyo WANAFUNZI hufundishwa Kristo ameteswa na kufufuka siku ya tatu na kwa sababu hiyo wapokee (watubu) na kuamini juu ya ONDOLEO la DHAMBI zao kwa KUFA NA KUFUFUKA kwa Yesu Kristo.
Hiki ndicho alichosema malaika na si kitu kingine..
Mathayo 1:21
[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.
Ndicho pia alichoandika Yohana kwa habari ya Agizo Kuu.
Yohana 20:21-23
[21]Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami NAWAPELEKA NINYI.
[22]Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu.
[23]Wo wote MTAKAOWAONDOLEA DHAMBI, WAMEONDOLEWA; na wo wote MTAKAOWAFUNGIA dhambi, WAMEFUNGIWA.
Watu wengine wakisoma hivi wanadhani kwamba Yesu ….

alimaanisha kuwa unakwenda tu kwa watu halafu unawaondolea dhambi labda kwa sababu zako mwenyewe na wengine unaaamua kuwaambia mmefungiwa dhambi zenu. Lakini sicho alichomaanisha Bwana wetu.
Haya ni matokeo ya kuhubiri injili. ANAYEPOKEA INJILI ANAPOKEA ONDOLEO LA DHAMBI, LAKINI ANAYEKATAA INJILI HUYO DHAMBI YAKE INAKAA. ANGALIA. Marko alivyosema *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*

Yohana pia ameandika.. Yohana 3:16-18
[16]Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
[17]Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.
[18]Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

Kwa hiyo WATU WANAAMINI KWA KUHUBIRIWA INJILI NA WANAHUKUMIWA KWA KUKATAA INJILI.

UKIANGALIA MSISITIZO WA YESU, SIYO KUWAAMBIA TU HABARI KISHA UNAONDOKA ZAKO BALI **KUWAFANYA WAWE WANAFUNZI. WANAFUNZI NI WATU AMBAO WANAKAA DARASANI KUFUNDISHWA.**

# KWA NINI UWAFANYE WENGINE KUWA WANAFUNZI?

Mambo uliyojifunza kwa muda wa wiki 10 kisha ndiyo ukaelewa, unafikiri ukiwaeleza watu wengine kwa sentensi moja wataelewa?

Ndiyo maana ni vizuri zaidi kubeba moyo wa ualimu (kuelezea kwa undani) kuliko kutegemea nukuu yako moja itawafanya watu waelewe.

Jifunze kutumia Mistari ya kutosha kuelezea jambo hilo kwa watu ambao wanasikia hivyo kwa mara ya kwanza.

Ijapokuwa haizuii moja kwa moja kuonekana umepotea lakini yafaa sana wewe kufanya assignment yako kama Mwalimu.

Kama unaandika kwenye status, elezea mpaka uone mtu anayefuatilia atakuwa ameelewa, kama unaweza andika hata article ndefu.. utawasaidia sana hasa wale ambao mioyo yao iko tayari kupokea.

Wakati mwingine ujizuie kusema mambo mengi mapya kwa wakati mmoja au session moja badala yake komaa na jambo moja baada ya lingine. USIOGOPE kuonekana una Mistari mingi. Usione shida kutumia mifano ya kutosha.

Usirukie jambo moja ukanukuu, ukarukia lingine.

Mpaka unamaliza dakika 10 ndugu msikilizaji anaumwa kichwa na hana alichoondoka nacho.

Tukumbuke ya kuwa sehemu kubwa ya watu tunaowahubiria tayari wanazo taarifa za Mungu hata kama siyo sahihi kwa hiyo hilo shamba ni la kung'oa huku unapanda.

# PATA MUDA KUELEZEA KUTOKA KWENYE MAANDIKO

(Moyo wa UANAFUNZI)

Inapofika kwenye swala la UANAFUNZI (discipleship) hakuna kitu kina nguvu kama kufungua maandiko.  Acha story zako za nilikuwa MLEVI sasa nimeacha, nilikuwa nakula wali sasa pilau... Fungua maandiko, mweleze utimilifu wa ahadi ya ukombozi wa mwanadamu katika maandiko. Hiyo ndiyo ndiyo namna ya Bwana wetu Yesu Kristo na ndiyo walikochukulia mitume na wewe pia unatakiwa kufuata mtindo huo huo.

Angalia mkazo wa Yesu ni Kufa na kufufuka kwake na matokeo yake ambayo ni UZIMA WA MILELE,  KUHESABIWA HAKI, MSAMAHA WA DHAMBI/KUONDOLOEWA AU KUFUTIWA DHAMBI, KUFANYWA MWANA WA MUNGU AMA KIUMBE KIPYA.

Kweli inakaa maeneo hayo,  mtu asipovuka hapa ameshaacha daraja na huko aendako atapotea.

Angalia Yesu alivyowaambia MITUME wake..

Luka 24:46-47

[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;

[47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

Kufa na kufufuka kwake na watu wahubiriwe habari ya toba ILETAYO ondoleo la Dhambi.

Angalia Petro... Matendo ya Mitume 2:32,38

[32]Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.

[38]Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Ni toba iletayo ondoleo la dhambi kwa kuamini kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Angalia sehemu nyingine akihubiri... Matendo ya Mitume 3:18-19

[18]Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.

[19]Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;

Watu watubu (waamini au wamgeukie) kwamba kwa njia ya Mauti yake wanapata ondoleo la dhambi.

Petro akiwa kwa Kornelio... Matendo ya Mitume 10:39-43

[39]Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini.

[40]Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika,

[41]si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu.

[42]Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.

[43]Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.

Kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.. kwa hiyo kule kutubu ni KUAMINI katika MAUTI yake na kufufuka kwake..

Paulo anafafanua Zaburi ya Daudi juu ya kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.. Matendo ya Mitume 13:28-30,32-39

[28]Na ijapokuwa hawakuona sababu ya kumfisha wakamwomba Pilato auawe.

[29]Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini.

[30]Lakini Mungu akamfufua katika wafu;

[32]Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,

[33]ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili,

Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.

[34]Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi,

Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.

[35]Kwa hiyo anena na pengine,

Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.

[36]Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.

[37]Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.

[38]Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;

[39]na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.

AMWAMINIYE HUHESABIWA HAKI...

Paulo tena .... Matendo ya Mitume 17:2-3

[2]Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu,

[3]akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.

## KRISTO KUTESWA, na KUFUFUKA KATIKA WAFU.

Paulo akiwa Rumi... Matendo ya Mitume 28:23

[23]Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu asubuhi hata jioni.

Paulo hapa alikuwa anashawishi kwa maandiko mengi, kuonya pale ni (expounding) yaani kufanya uchambuzi wa vitabu vya Musa na manabii KUWAONYESHA habari za Ukombozi wa mwanadamu katika Kristo Yesu. Tena kwa TARATIBU, ASUBUHI MPAKA JIONI.

Ndugu zangu, usione shida kuonekana Mwalimu sana. Fungua maandiko, elezea maandiko usikubali hadithi za kidini..

waonyeshe ahadi ya Mungu iliyotimizwa tena iliyo wazi katika maandiko.

## KRISTO AUMBIKE NDANI YAO.

Huo ndio moyo wa UANAFUNZI. FUNGUA MAANDIKO.

So, Reach Out And Disciple (R.O.A.D). Are you doing it?

# UANAFUNZI NI MAHUSIANO

Hebu fikiri Yesu na huduma yake.. alitumia muda kuwalea kwa kuwafundisha wanafunzi wake siyo kwa siku mbili siyo kwa kuwaambia kisha waende wajitafute huko mbele.. ALIWEKEZA MUDA.. Hata pale ambapo bado walikuwa wanaonyesha kupwaya, baada ya kufufuka akaendelea kuwathibitisha yale aliyowaambia.. na kuwafundisha kwa muda wa siku 40.

Angalia mwenyewe... Luka 24:36-48

[36]Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu.

[37]Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho.

[38]Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu?

[39]Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.

[40]Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake.

[41]Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa?

[42]Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa.

[43]Akakitwaa, akala mbele yao.

[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.

[45]Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.

[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;

[47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

[48]Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.

Haya mambo ya KUWAFUNULIA MAANDIKO SIYO KUWAWEKEA MIKONO NI KUWAELEZEA MPAKA WASEME "AHAA SASA NIMEELEWA".

Matendo ya Mitume 1:3

[3]wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu.

Petro naye.. Matendo ya Mitume 2:40-42

[40]Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.

[41]Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.

[42]Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.

Baada ya kuwashuhudia kwa Maneno mengi sana HATA hivyo WALIENDELEA KUDUMU KATIKA FUNDISHO.

Matendo ya Mitume 19:7-10

[7]Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili.

[8]Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu.

[9]Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano.

[10]Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani.

HAO WANAFUNZI PAULO ALIKOMAA NAO ZAIDI YA MIAKA MIWILI.... Yaani kuhakikisha kuwa wameiva.

UANAFUNZI UNA GHARAMA YAKE KWA MWALIMU NA MWANAFUNZI.

Ni afadhali ukomae na watu 10 hadi waweze kuwakomaza wengine 10 kuliko kukimbiakimbia na watu 200 ambao hawajaelewa chochote wanabebwa na kila upepo ujao.

DISCIPLESHIP IS RELATIONSHIP

INVEST IN TIME.

TAKE TIME. YES I SAY TAKE TIME.

# SIYO UBUNIFU, NI MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI

Kati ya njia rahisi kabisa ya kupotea kwenye njia ya kweli ni kujitahidi kubuni Injili tofauti na yale ambayo mitume wamefundisha.

That's the sure way to get lost.

Jicho lako likitoka kwenye kutazama kazi ya Mungu katika Kristo yaani Mateso ya Kristo na kuingia katika utukufu wake umeanza kugeukia hadithi za kizee.. na huo ni Mwanzo wa kupotea.

Musa, manabii na Zaburi au kwa lugha rahisi: Vitabu 39 vya Mwanzo mpaka Malaki, ujumbe wake kwa UMOJA ni KRISTO. Siyo tu Kristo lakini katika kupata mateso na utukufu uliofuata.

Hiyo ndiyo message ya maandiko matakatifu, hiyo ndiyo inabidi kuelezewa kwa usahihi wake tena kwa muda wa kutosha.

Paulo alimwambia Timotheo.. 2 Timotheo 2:2

[2]Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.

Sasa angalia hiyo RELAY...

Mambo aliyosikia kwake, AWAKABIDHI siyo afanye editing na kuwapa kitu kipya.. yaani ACHUKUE alichoambiwa na KUWAKABIDHI watu wengine WAAMINIFU yaani watu WALIOSIKILIZA KWA UAMINIFU YAANI WALIOKAA KUFUNDISHWA kisha na wao wawakabidhi WENGINE.

RELAY INAENDA HIVYO.. kwenye RELAY tunapokezana kijiti kimoja. No change.

Swali ni kwamba, Paulo Yeye alichukua wapi?

Jibu rahisi ALIFUNDISHWA NA MITUME, Kwanza alisikia wakati Stefano anahubiri na akisimamia tukio zima, na baada ya maono Anania alikwenda kuzungumza naye pia.

Hata alipopata hayo maono alikumbushwa juu ya yale aliyoyaona (bila shaka ni kwa Stefano).

Matendo ya Mitume 26:15-18

[15]Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi.

[16]Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako;

[17]nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao;

[18]uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.

Ili watu wapate Msamaha wa dhambi ni lazima wahubiriwe KAZI YA KRISTO YAANI MATESO YAKE NA KUFUFUKA KWAKE.

Kama Yesu alivyosema.. Luka 24:46-47

[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;

[47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

Hivyo ndivyo mitume walivyopokea kwa Yesu lakini pia Yesu hakutoa hewani bali kwenye vitabu vya Musa, Manabii na Zaburi. Angalia hapa.. Luka 24:44

[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.

Hii ni kazi ambayo Mungu aliishuhudia tangu kitambo, Tangu Mwanzo 1... Warumi 1:1-4

[1]Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu;

[2]ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu;

[3]yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili,

[4]na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu;

Injili ya Mungu ni Habari za MWANAWE, Kupata mateso, kufa na kufufuka.. huu ndiyo UJUMBE aliouhubiri Mungu tangu ZAMANI. Siyo ujasiriamali, siasa, uchumi, sanaa, muziki au vitu vinavyofanana na hivyo Bali AHADI YA UKOMBOZI KUPITIA MWANAWE YESU KRISTO.

Yesu alimwambia Kleopa na yule ndugu.. Luka 24:25-27

[25]Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!

[26]Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?

[27]Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

Paulo alimpa Timotheo Injili hiyo na Timotheo alitakiwa kuwapa watu WAAMINIFU pia nao wasikae nao bali WAWAFUNDISHE WENGINE..

Angalia Paulo alichohubiri kwenye Matendo ya Mitume 13:26-39

[26]Ndugu zangu, wana wa ukoo wa Ibrahimu, na hao miongoni mwenu wanaomcha Mungu, kwetu sisi neno la wokovu huu limepelekwa.

[27]Kwa maana wakaao Yerusalemu, na wakuu wao, kwa kuwa hawakumjua yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila sabato, wameyatimiza kwa kumhukumu.

[28]Na ijapokuwa hawakuona sababu ya kumfisha wakamwomba Pilato auawe.

[29]Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini.

[30]Lakini Mungu akamfufua katika wafu;

[31]akaonekana siku nyingi na wale waliopanda naye kutoka Galilaya hata Yerusalemu, ambao sasa ndio walio mashahidi wake mbele ya watu.

[32]Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa,

[33]ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili,

Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.

[34]Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi,

Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini.

[35]Kwa hiyo anena na pengine,

Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu.

[36]Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu.

[37]Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu.

[38]Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi;

[39]na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.

Ni kufa na kufufuka kwa Yesu na matokeo yake au kuamini hayo ni KUHESABIWA HAKI BURE.

Paulo anamchukua Timotheo.. Matendo ya Mitume 16:1

[1]Basi akafika Derbe na Listra, na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo, mwana wa mwanamke Myahudi aliyeamini; lakini babaye alikuwa Myunani.

Sura inayofuata Paulo anahubiri kwenye masinagogi... Matendo ya Mitume 17:2-3

[2]Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu,

[3]akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.

Angalia alichohubiri.. ILIMPASA KRISTO KUTESWA, NA KUFUFUKA KATIKA WAFU; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.

Hizo sabato 3 alikuwa anakomaa na maandiko yaani Mwanzo mpaka Malaki akionyesha hayo tu.

Alipokuwa KORINTHO alikuwa Sila na Timotheo. Angalia Matendo ya Mitume 18:4-5

[4]Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani.

[5]Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo.

Hii ni sawa na kuwaambia.. huyo Kristo aliyetabiriwa ni YESU.

TIMOTHEO ALIENDELEA KUAMBATANA NAYE.

Paulo akiwa Efeso ambapo ndipo mahali ambapo Timotheo alikuwa anahudumia... Paulo akiwa na wanafunzi 12... ambapo alikuwa anahudumu kwenye sinagogi AKIWA NAO.

Matendo ya Mitume 19:7-10

[7]Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili.

[8]Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu.

[9]Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano.

[10]Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani.

Baada ya Fujo akawakusanya sehemu akakaa kuwafundisha kwa muda wa miaka zaidi ya miwili.

Umeona alichohubiri Paulo?

Umeona alivyompasia Timotheo?

Umeona uaminifu wa Timotheo katika kujifunza?

Sasa ndugu yangu?

KUSIKIA SANA NDIYO INATAKIWA. YES. UJUMBE ULE ULE.. KRISTO.  SIKIA KUTOKA PANDE ZOTE za KIUCHAMBUZI  WA KIMAANDIKO.

Ukiona unachoka kusikia habari za Kristo ujue masikio ya utafiti yanakusumbua.. utaambulia mafundisho potofu.

Baki na Kristo.  Huwezi kuwa zaidi ya Petro na Paulo

# KUAMUA KUHUBIRI KWELI NI KUAMUA KUTOHUBIRI KITU KINGINE

TO CHOOSE THE GOSPEL IS TO RESTRAIN FROM COMPROMISING

Sauti ni nyingi sana ambazo siyo Injili, mvutano wa kusema "kinyume" na Injili ya nao pia upo. Mitume hawaagizi tu INJILI ihubiriwe lakini pia kujizuia (restrain) kuhubiri kitu kingine.

Hivi ni  vita hasa katika UANAFUNZI.  Si ajabu mtu ajabu leo mtu anarukaruka kuelewa Injili kesho anaanza kupiga mabokolikolo.□

The gospel is a "what to do" coming with a "what not to do".

Paulo anastaajabu kwamba kanisa  Galatia limeanza kula mambo mengine tofauti na Injili. Angalia Wagalatia 1:6-8

[6]Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine.

[7]Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo.

[8]Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.

Neno alaaniwe pale ni anathema ambayo maana yake siyo kulaani AFE lakini kupata "BAN" yaani asipewe nafasi, ANYIMWE, ABANIWE ☐. Wawe excommunicated.. wanyimwe nafasi kabisa.

This is serious.

Ndiyo maana Yohana alisema 2 Yohana 1:9-11

[9]Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.

[10]Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu.

[11]Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu.

Huyu ndugu asipewe jukwaa, usimtegee sikio, msimpe ushirikiano kabisa.

Lakini kwenye kuonya kwamba mtu mwingine asihubiri kitu kingine anaanza kwa kusema "SISI" kwa sababu hata Yeye anatakiwa kuwa na adabu ya kutovutiwa kuhubiri kitu kingine abaki na Injili ya Kweli.

Angalia alivyosema kwenye Matendo ya Mitume 26:22-23

[22]Basi kwa kuwa nimeupata msaada utokao kwa Mungu nimesimama hata leo hivi nikiwashuhudia wadogo kwa wakubwa, WALA SISEMI NENO ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa;

[23]ya kwamba Kristo hana budi KUTESWA NA YA KWAMBA YEYE KWANZA KWA KUFUFULIWA KATIKA WAFU ATATANGAZA HABARI ZA NURU KWA WATU WAKE NA KWA WATU WA MATAIFA.

Hasemi kitu kingine.. ila yale ambayo manabii (katika Mwanzo Mpaka Malaki) wamesema kama AHADI kuwa Kristo atateswa na kufufuka kisha atatangaza habari za nuru yaani UKOMBOZI WA MWANADAMU KUTOKA KWENYE DHAMBI ndiyo kusema kupata uzima wa milele au Msamaha wa dhambi/ondoleo la dhambi/KUHESABIWA HAKI au Mwanadamu na Mungu kuwa pamoja (roho moja milele).

Huko kusema HASEMI maana yake alikuwa ka uwezo wa kusema mambo mengi alibaki na Injili "sticking to the message".

Hayo MAAGIZO anampa Timotheo pia kuwa AWAKATAZE watu wasifundishe kitu kingine kwenye maandiko. Hii ina maana watu wanaweza kusoma maandiko badala ya kukutana na Injili ya Yesu Kristo kupata mateso, Kufa na kufufuka na habari njema za mambo hayo wanaishia kukutana na elimu nyingine na hadithi..

1 Timotheo 1:3-4

[3]Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine;

[4]wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani; basi ufanye hivyo.

Shida ya kwamba mambo hayo hayaleti MADARAKA YA MUNGU YALIYO KATIKA IMANI.

Hayo mambo aliyowaambia UWAKATAZE wasifundishe kwa sababu hayaleti madaraka ya Mungu yaliyo katika imani kwenye sura ya nne anayaita MAFUNDISHO YA MASHETANI.

1 Timotheo 4:1

[1]Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;

Mafundisho ya MASHETANI siyo ETI, NAMNA YA KUJIUNGA FREEMASON AU NAMNA YA KUMSUJUDU SHETANI bali ni usomaji na tafsiri ya maandiko matakatifu unaopingana na YALE AMBAYO KRISTO amefanya kwa KUPATA MATESO, KUFA NA KUFUFUKA KWAKE. Kwa mfano kwenye sura ya nne ni LEGALISM (Kukataza watu kuoa na kula).

1 Timotheo 4:2-3

[2]kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe;

[3]wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli.

Kwa hiyo mtu akitumia maandiko kufundisha aina za wanyama wa kula na kutokula ni Matumizi mabaya ya maandiko matakatifu na ndiyo MAFUNDISHO YA MASHETANI.

Hii ni kwa sababu JUMLA YA FUNDISHO LINALOPATIKANA KWENYE MWANZO MPAKA MALAKI NI KRISTO KATIKA KUPATA MATESO NA KUFA PAMOJA NA KUFUFUKA KWAKE. Hicho ndicho unachotakiwa kuona.

Angalia Yesu alivyosema

Luka 24:25-27

[25]Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!

[26]Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?

[27]Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

Tena akaongezea katika Luka 24:44,46-47

[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.

[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;

[47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

Hii ndiyo SUMMARY ya Agano la Kale... kujitahidi kuona nje ya Kristo ni hakika ya kupata MAFUNDISHO YA MASHETANI.

Yaani pale unaposoma Habari za Yusufu wewe unaona mbinu za kufikia maono Yakobo, Habakuki na namna ya kuandika njozi, Musa na namna ya kuvuka jangwani, Habili na namna ya kuwaepuka watu wenye chuki, ni KUPOTEA KABISA.. Ni kupata mafundisho ya MASHETANI.

Ndiyo maana kwa habari ya vitabu vya Musa Yesu anasema wazi kwamba vinamhusu YEYE..

ANGALIA Yohana 5:39-40,45-46

[39]Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.

[40]Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.

[45]Msidhani kwamba mimi nitawashitaki kwa Baba; yuko anayewashitaki, ndiye Musa, mnayemtumaini ninyi.

[46]Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu.

Musa anachoandika huko Mwanzo, siyo uumbaji, unajimu, wanyama, mimea, matunda wala ndoa... bali ni habari za Yesu Kristo kwa kutumia lugha hizo hizo za viumbe na matukio.

Kwa hiyo namna Paulo alivyomfunua Kristo katika maandiko anamwambia Timotheo aliyekuwa mwaminifu katika kusikiliza awakabidihi na watu (kwa kufundisha) ili nao wawakabidhi watu wengine waaminifu na MNYORORO utaendelea.

2 Timotheo 2:2

[2]Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.

Kule kuwaambia MAMBO YALE ULIYOYASIKIA ni sawa na Kusema USIHUBIRI AU KUFUNDISHA MAMBO MENGINE NA HAO WENGINE UWAKATAZE PIA WASIHUBIRI MAMBO MENGINE.

Yes, watu waaminifu wanasikiliza ujumbe ule ule na kuwaambia wengine ujumbe huo huo. Na hii ni kwa sababu changamoto ni watu kutaka kusikiliza vitu vipya ambavyo siyo kwa namna ya

Kristo. Paulo anamwagiza Timotheo tena katika 2 Timotheo 4:1-4

[1]Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake;

[2]lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.

[3]Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti;

[4]nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.

Anamwagiza akomae na mafundisho huko akiwa alert kwamba wadau huo wanachokaga na kutaka msosi mpya.

Mtu mmoja aliwahi kumwambia mtumishi "YAANI WEWE KILA SIKU KRISTO TU?"

Kule kusema WATAYAKATAA MAFUNDISHO YENYE UZIMA kwa Kingereza wanasema THEY WILL NOT ENDURE (KJV) Maana yake watashindwa kuvumilia.. watakata kutest zari jipya...

Ni UVUMILIVU kumwona Kristo Yesu mwanzo mpaka mwisho wa maandiko matakatifu. Watu wanawashwa masikio, wanataka

kusikia kitu kipya.. na HABARI MBAYA NI KWAMBA WATAFANIKIWA KUJIEPUSHA KUSIKIA YALIYO KWELI NA KUGEUKIA HADITHI ZA UONGO (fables or tuition)..

Ndugu yangu komaa na Kristo acha hizo TUITION ZA PEMBENI ZA KUCHAMBUA MAANDIKO KWA NAMNA ISIYO YA KRISTO. UNACHOKITAFUTA UTAKIPATA ILI KILICHOKUSUDIWA NA MUNGU KWENYE MAANDIKO UTAKIKOSA and that's not BEING SMART AT ALL.

BE SMART.

LEARN CHRIST,

SHARE CHRIST.

# WAAMBIE WATU WOTE UJUMBE HUO HUO

Injili ni ujumbe mmoja wa Mungu unaozungumzia WOKOVU kwa wanadamu. Ni ujumbe usiobadilika kulingana na aina ya watu wasikiao au mazingira yaliyopo.

Hauna sura tofauti mbele ya masikini na tajiri,  haina tofauti mbele ya wasomi na wasio na elimu, mbele ya akina baba na akina mama. Hauangalii rangi au jinsia ya mtu.. ujumbe ule ule unampa balozi wa nyumba kumi na raisi wa nchi... ndio huo huo utampa mwanasiasa na mtu asiye na cheo chochote.

Ukishabadilika... huo siyo ujumbe wa Mungu na kwa maana hiyo siyo Injili.

Angalia.. Paulo anasema jinsi alivyofanya alipokuwa KORINTHO..

1 Wakorintho 2:1-2

[1]Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima.

[2]Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa.

PAULO HAKUTAKA AZUNGUMZIE KITU KINGINE CHOCHOTE KAMA INJILI IJAPIKUWA KUNA MAMBO MENGI HUKO KORINTHO ILA ALIKOMAA NA YESU KRISTO ALIYESULUBIWA.

Petro mbele ya WATU WA AINA MBALIMBALI... Matendo ya Mitume 2:5,32,38-39,41

[5]Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.

[32]Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.

[38]Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

[39]Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.

[41]Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.

PETRO HAKUSEMA KWA SABABU WATU HAWA NI JAMII MBALIMBALI NGOJA NITAFUTE MAMBO FULANI YA KUSEMA ILA ALICHAMBUA MAANDIKO AKIONYESHA KUWA KRISTO ALISULUBIWA, AKAFA

NA AKAFUFUKA NA KWA AJILI HIYO WAPATE KUTUBU (KUMGEUKIA) WAOKOLEWE.

Petro mbele ya HEKALU, hakujifanya kusema Aah hawa watu wanasomaga Torati na manabii watakuwa wanaelewa. Hapana. Alihubiri kitu alichohubiri Matendo ya mitume 2.

Angalia.. Matendo ya Mitume 3:18-24

[18]Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo.

[19]Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;

[20]apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani;

[21]ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.

[22]Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.

[23]Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.

[24]Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.

KUFA NA KUFUFUKA KWAKE NA MATOKEO YA KUAMINI HILI TU..

Alipokuwa mbele ya BARAZA... mbele ya watu "wakubwa" hakuchapia au kuleta ujumbe mpya.. alikomaa na Habari ile ile...

Matendo ya Mitume 4:8-12

[8]Ndipo Petro, akijaa Roho Mtakatifu, akawaambia, Enyi wakubwa wa watu na wazee wa Israeli,

[9]kama tukiulizwa leo habari ya jambo jema alilofanyiwa yule mtu dhaifu, jinsi alivyoponywa,

[10]jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu.

[11]Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni.

[12]Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.

Ni kitu kile kile... WOKOVU KATIKA JINA LA YESU KRISTO (KUFA NA KUFUFUKA KWAKE).

Filipo mbele ya towashi mtu mwenye CHEO.. hakuanza kumsifia wala kumpamba.. alianza kumhubiri KRISTO..

ANGALIA

Matendo ya Mitume 8:26-35

[26]Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa.

[27]Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu,

[28]akawa akirejea, ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya.

[29]Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo.

[30]Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma?

[31]Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye.

[32]Na fungu la Maandiko alilokuwa akilisoma ni hili,

Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo,

Na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya,

Vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake.

[33]Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa.

Ni nani atakayeeleza kizazi chake?

Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi.

[34]Yule towashi akamjibu Filipo, akasema, Nakuomba, nabii huyu; asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine?

[35]Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu.

HABARI NJEMA ZA YESU SIYO KITU KINGINE BALI NI KUFA NA KUFUFUKA KWAKE NA MATOKEO YAKE KWA MWANADAMU, NA AKAAMINI..

Petro mbele ya Kornelio, AFISA WA JESHI.. Hakuanza kubwabwaja na kutunga mambo ya kusema, hata kama afisa ana

maono kama yote, anaongea na malaika.. AKAKOMAA NA UJUMBE ULE ULE.. Siyo unakutana na mtu anakwambia jana niliambiwa mtakuja kwenye maono unaanza kumwomba Yeye ndo akuhubirie. Wewe hubiri wewe wala usibadili ujumbe. Unaweza kuwa na maono na hujaamini.

Angalia Petro, Matendo ya Mitume 10:1-2,34-44

[1]Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia,

[2]mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima.

[34]Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo;

[35]bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.

[36]Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote),

[37]jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianzia Galilaya, baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana;

[38]habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.

[39]Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini.

[40]Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika,

[41]si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu.

[42]Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu.

[43]Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.

[44]Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno.

Yes, alihubiri toba iletayo ondoleo la dhambi na Wakajazwa na Roho Mtakatifu.

Imagine angebadili ujumbe..

Paulo aliend mji wenye watu wenye elimu zao, za dini tofauti tofauti, mji uliojaa sanamu na masinagogi.. UJUMBE WAKE AKAUVUTA KULE KULE.. Hakuanza na HASARA 50 ZA KUABUDU SANA.. BALI ALIMLETA KRISTO KWENYE MWANGA.

ANGALIA Matendo ya Mitume 17:16-32

[16]Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.

[17]Basi katika sinagogi akahojiana na Wayahudi na waliomcha Mungu, na wale waliokutana naye sokoni kila siku.

[18]Na baadhi ya Waepikureo na Wastoiko, wenye ujuzi, wakakutana naye. Wengine wakasema, Mpuzi huyu anataka kusema nini? Wengine walisema, Anaonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni, kwa maana alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufufuo.

[19]Wakamshika, wakamchukua Areopago, wakisema, Je! Twaweza kujua maana ya elimu hii mpya unayoinena?

[20]Kwa maana unaleta mambo mageni masikioni mwetu, tutapenda kujua, basi, maana ya mambo haya.

[21]Kwa maana Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lo lote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya.

[22]Paulo akasimama katikati ya Areopago, akasema, Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini.

[23]Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua.

[24]Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono;

[25]wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.

[26]Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao;

[27]ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu.

[28]Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema, Maana sisi sote tu wazao wake.

[29]Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu.

[30]Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.

[31]Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.

[32]Basi waliposikia habari za ufufuo wa wafu wengine walifanya dhihaka; wengine wakasema, Tutakusikiliza tena katika habari hiyo.

ALIKOMAA NA KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU HATA KAMA WALIBEZA.. THE MESSAGE IS STILL THERE.

Ukiona kila aina ya watu unaokutana nao una jumbe ambazo tofauti tofauti za kuwapa ili WA FIT VIZURI KWENYE HUO UJUMBE... HIYO SIYO INJILI..

INJILI NI SPECIFIC.

Injili ya kweli haichagui mtu!..

Kama masikini wanaweza KUPOKEA na matajiri HAWAWEZI hiyo siyo Injili.

Kama Watanzania wataelewa halafu halafu ukifika kwa Wamarekani unabadilisha ujumbe hiyo siyo Injili.

Kama UKIWAAMBIA wanawake wanapokea lakini ikawabagua wanaume hiyo siyo Injili.

Kama mabosi wanaelewa lakini wafanyakazi hawaelewi hiyo siyo Injili.

Kama mtu mwenye matendo mabaya atapokea lakini mwenye matendo mema ataona hayamhusu hiyo siyo Injili.

Injili ya kweli ni CROSS CULTURAL, CROSS BORDERS, CROSS STATUSES.

ALL MEN NEED IT!.

Now you can see if you're preaching the GOSPEL OF JESUS CHRIST OR GOSSIPING OF MEN.

# HAINA MAANA WOTE WATAKUBALI

Jambo la kwanza kabisa Mhubiri wa Injili anatakiwa kupona ni kutofikiri ya kwamba  kwa sababu yuko sahihi kila mtu atasema NDIYO. Hiyo haina guarantee kwa sababu kuamini ni ushawishi wa Roho juu ya mioyo ya watu, wakati huo huo watu wengine wanaweza kukataa huo ushawishi kabisa, wengine kwa kitambo au wengine kwa kupata muda wa kuhakiki yale unayoyasema kwa kina.

Usichukulie kukataliwa kwa ujumbe kwamba kuna kitu hakiko sawa kwako au kwenye namna ulivyowasilisha. Siyo mara zote unakuwa umekosea.

Yesu alisema mapema kabisa kwa wanafunzi.

Yesu aliwapa maelezo ya kina juu ya mazingira ya Injili.. inaweza isiwe SHWAAARI.. Inaweza kuwa na misukosuko..

Yohana 15:18-27

[18]Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi.

[19]Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia.

[20]Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu.

[21]Lakini haya yote watawatenda kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyenipeleka.

[22]Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao.

[23]Yeye anichukiaye mimi humchukia na Baba yangu.

[24]Kama nisingalitenda kwao kazi asizozitenda mtu mwingine, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa wametuona mimi na Baba yangu, na kutuchukia.

[25]Lakini litimie lile neno lililoandikwa katika torati yao, Walinichukia bure.

[26]Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia.

[27]Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami.

Akaendelea kwenye Yohana 16:1-4

[1]Maneno hayo nimewaambia, msije mkachukizwa.

[2]Watawatenga na masinagogi; naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ya kuwa anamtolea Mungu ibada.

[3]Na hayo watawatenda kwa sababu hawakumjua Baba wala mimi.

[4]Lakini nimewaambia hayo, ili makusudi saa ile itakapokuja myakumbuke ya kuwa mimi naliwaambia.

Kwa hiyo mitume walikuwa hawaoni ajabu kupingwa, kupigwa na kudhalilishwa... Wanamchukia uliyembeba, wanachukia ujumbe wako.. HIYO YATOSHA KUWA SABABU YA WEWE KUCHUKIWA..

Pamoja na kufanya ishara na miujiza kibao bado walipingwa na kupigwa..

Matendo ya Mitume 5:40-42

[40]Wakakubali maneno yake; nao walipowaita mitume, wakawapiga, wakawaamuru wasinene kwa jina lake Yesu; kisha wakawaacha waende zao.

[41]Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo.

[42]Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.

Ishu ni kwamba hawakuacha.. waliendelea mbele.. kusema na kutenda walichoagizwa. Na walifurahia hata mateso yao katika hali hiyo.

Ndugu yangu, kama unatafuta KUKUBALIKA NA WATU, INJILI SIYO MAHALI SAHIHI KWAKO. HUKU KUKATALIWA NI PACKAGE.  Pamoja na kupingwa, kupigwa na kukatawaliwa huoni mitume wakifanya maombi kuzuia ROHO YA KUKATALIWA ila UJASIRI..

Angalia... Matendo ya Mitume 4:29-31

[29]Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote,

[30]ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu.

[31]Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

Yes. Ujasiri na ishara..

Stefano alipokuwa anahubiri...

Matendo ya Mitume 6:8-15

[8]Na Stefano, akijaa neema na uwezo, alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katika watu.

[9]Lakini baadhi ya watu wa sinagogi lililoitwa sinagogi la Mahuru, na la Wakirene, na la Waiskanderia, na la wale wa Kilikia na Asia, wakaondoka na kujadiliana na Stefano;

[10]lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye.

[11]Hata wakashawishi watu waliosema, Tumemsikia mtu huyu akinena maneno ya kumtukana Musa na Mungu.

[12]Wakawataharakisha watu na wazee na waandishi, wakamwendea, wakamkamata, wakampeleka mbele ya baraza.

[13]Wakasimamisha mashahidi wa uongo waliosema, Mtu huyu haachi kusema maneno ya kufuru juu ya mahali hapa patakatifu na juu ya torati;

[14]maana tumemsikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa.

[15]Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika

Mbali na kuwa na neema na uwezo, lakini walitafuta njia ya kumtengenezea ZENGWE hata kwa kutumia mashahidi wa uongo..

Lakini wote tunajua kilichompata Stefano baada ya kuendelea kuhubiri kweli..

Matendo ya Mitume 7:57-60

[57]Wakapiga kelele kwa sauti kuu, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa nia moja,

[58]wakamtoa nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi wakaweka nguo zao miguuni pa kijana mmoja aliyeitwa Sauli.

[59]Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu.

[60]Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.

Na Stefano bado hakuwa na uchungu na wale waliomuua. Bali aliwaombea na Sauli alikuwa akiona kila kitu.

Hata Sauli baada ya kubadilika moja kwa moja akaanza kuwa adui na yeye.. akatafutwa kuuawa.

Angalia Matendo ya Mitume 9:20-22

[20]Mara akamhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.

[21]Na wote waliosikia wakashangaa, wakasema, Siye huyu aliyewaharibu walioliitia Jina hili huko Yerusalemu? Na hapa alikuwa amekuja kwa kusudi hilo, awafunge na kuwapeleka kwa wakuu wa makuhani?

[22]Sauli akazidi kuwa hodari, akawatia fadhaa Wayahudi waliokaa Dameski, akithibitisha ya kuwa huyu ndiye Kristo.

Alipoanza tu Injili... Matendo ya Mitume 9:23-25

[23] Hata siku nyingi zilipopita, Wayahudi wakafanya shauri ili wamwue;

[24]lakini hila yao ikajulikana na Sauli. Wakamvizia malangoni mchana na usiku wapate kumwua.

[25]Wanafunzi wake wakamtwaa usiku wakamshusha ukutani, wakimtelemsha katika kapu.

Mbali na kwamba Sauli alikoswakoswa.. Yakobo aliuawa...

Matendo ya Mitume 12:1-2

[1]Panapo majira yale yale Herode mfalme akanyosha mikono yake kuwatenda mabaya baadhi ya watu wa kanisa.

[2]Akamwua Yakobo, ndugu yake Yohana, kwa upanga.

Lakini Petro naye alikuwa auawe kanisa likaomba.. Matendo ya Mitume 12:5

[5]Basi Petro akalindwa gerezani, nalo kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake.

Na matokeo yake ni kuokolewa na mkono wa Herode.

Paulo alipigwa Listra hadi walidhani ameshakufa... Matendo ya Mitume 14:19

[19]Lakini Wayahudi wakafika toka Antiokia na Ikonio, wakawashawishi makutano hata wakampiga kwa mawe Paulo, wakamburuta nje ya mji, wakidhania ya kuwa amekwisha kufa.

Paulo alipokuwa Thesalonike wengine walikubali na wengine walikataa, siyo kukataa tu ila na Wayahudi waliandaa "mob" wahuni wawashughulikie na Yasoni aliyewapokea hakuwa salama pia. Matendo ya Mitume 17:2-9

[2]Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu,

[3]akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo.

[4]Wengine miongoni mwao wakaamini, wakashikamana na Paulo na Sila; na Wayunani waliomcha Mungu, wengi sana, na wanawake wenye cheo si wachache.

[5]Na Wayahudi wakaona wivu, wakajitwalia watu kadha wa kadha katika watu ovyo wasio na sifa njema, nao wakakutanisha mkutano, wakafanya ghasia mjini, wakawaendea watu wa nyumba ya Yasoni, wakataka kuwapeleka mbele ya watu wa mji;

[6]na walipowakosa, wakamkokota Yasoni na baadhi ya ndugu mbele ya wakubwa wa mji, wakipiga kelele, wakisema, Watu hawa walioupindua ulimwengu wamefika huku nako,

[7]na Yasoni amewakaribisha; na hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume cha amri za Kaisari, wakisema na kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu.

[8]Wakafadhaisha ule mkutano na wakubwa wa mji walipoyasikia hayo.

[9]Nao walipokwisha kumtoza dhamana Yasoni na wenziwe wakawaacha waende zao.

Hayo yote ni mambo ya kusingiziwa.

Kwa sababu ya Injili.

Dhihaka haikuwa kidogo pia kwa Paulo.. angalia Matendo ya Mitume 17:31-34

[31]Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.

[32]Basi waliposikia habari za ufufuo wa wafu wengine walifanya dhihaka; wengine wakasema, Tutakusikiliza tena katika habari hiyo.

[33]Basi hivi Paulo akaondoka akawaacha.

[34]Baadhi ya watu wakashikamana naye, wakaamini; katika hao alikuwamo Dionisio, Mwareopago, na mwanamke mmoja jina lake Damari, na watu wengine pamoja na hao.

Habari njema ni kwamba kuna watu walioamini..

Paulo akiwa KORINTHO hakupigiwa makofi na kila mtu.. Matendo ya Mitume 18:4-6

[4]Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani.

[5]Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo.

[6]Walipopingamana naye na kumtukana Mungu, akakung'uta mavazi yake, akawaambia, Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi; tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa.

WALIPINGANA NA KUMTUKANA MUNGU.

Hata alipofika Efeso nako.. Matendo ya Mitume 19:9

[9]Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano.

Hawa WALIKAIDI, WAKAKATAA KUAMINI NA KUITUKANA NJIA ILE (IMANI) MBELE YA WATU WOTE.

Paulo angetosha kusema ENOUGH IS ENOUGH. Nawaombea wafe au pengine hii kitu si sawa au mmmh au sijaitwa nini?

Acha hayo mawazo..

Wewe mwenzangu UNAHUBIRI nini? Kila mtu anakupigia makofi? Kila media inakukubali? Ni congratulations tu Mwanzo hadi mwisho.

Ulipoanza kuhubiri, ukagundua kuna watu kwenye cycle yako wamepungua, umeona LIKE NA WATU WANAKU UNFOLLOW INSTAGRAM, Unataka kurudi kufundisha mambo ya kuvutia nyomi? Umeona viewers wamepungua unataka kulegeza kamba, unataka kuchanganya kidogo na kakitu cha kuwa keep audience.

Mwisho kabisa.. niseme... Tuendelee kuomba kwa ajili ya UJASIRI, ULINZI NA KWAMBA NENO LIENDELEE.

2 Wathesalonike 3:1-2

[1]Hatimaye, ndugu, tuombeeni, neno la Bwana liendelee, na kutukuzwa vile vile kama ilivyo kwenu;

[2]tukaokolewe na watu wasio haki, wabaya; maana si wote walio na imani.

# MWISHO

KWA AJILI YA KUPATA MAFUNDISHO ZAIDI

TUMA JINA LAKO KWA WHATSAPP +255 714 548 565

AU INGIA KWENYE YOUTUBE CHANNEL YA Apostle Shemeji Melayeki (LINK) https://www.youtube.com/channel/UCzbLDMKAORgoLhM_77Z2zJQ

AU WEBSITE YA GLOBAL FAMILY GATHERINGS https://globalfamilygatherings.co.tz/

Umebarikiwa.